Responsible Mining Foundation

Chombo cha uchunguzi ya eneo ya ku chimba madini

Jina ya eneo ya madini:	
Jina ya kampuni:	
Fasi:	
Siku:	

01 Ku usu wafanyakazi wana mujini

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha hazarani wafanyakazi ngapi ku tokeya jami zinayo ishi eneo kampuni ina chimba madini?	☐	☐
b.	Ya julisha wafanyakazi ngapi wanao tokeya jami zinayo ishi eneo kampuni ina tumika wenyi kutumikishwa kupitiya wa sous-traitants?	☐	☐
c.	Ya julisha wafanyakazi ngapi wa kike ku tokeya jami zenyi ku ishi eneyo kampuni ina tumika wa nao i tumikiya ao wanao tumikiya wa sous- traitants za kampuni ?	☐	☐
d.	Ya julisha wafanya kazi wake na wanaume ngapi wenyi ku itumikia ama kutumikia sous-traitant tokea jami za eneo ime tumika walio pata cheo za juu?	☐	☐

02 Ku nunuwa kwenyi eneo

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni :	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha franka inayo i tumiya kwa ku nunuwa vifaa za kazi?	☐	☐
b.	Ya julisha vifaa za kazi zenyi ina nunuwa katika eneo iyo?	☐	☐
c.	Ya shirikisha ao ya husisha jamii zenyi ku ishi eneo za kazi zake ndani ya mipango zaku nunuwa vifaa za kazi?	☐	☐
d.	Ya husisha kabisa wanawake ku tokeya jamii zenyi ku ishi eneo za kazi zake ndani ya mipango zaku nunuwa vifaa za kazi?	☐	☐

03 Hali ya hewa

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha mara kwa mara hali ya hewa kwa kila sehemu ya ufatiliyaji ama surveillance?	☐	☐
b.	Ya julisha wakati gani na sehemu gani hali ya hewa ina shuka chini ya mupaka ya usalama?	☐	☐
c.	Ya husisha ama ya shirikisha jamii zinayo ishi eneo za kazi katika ku kamata atuwa yaku linda hali ya hewa?	☐	☐
d.	Ya husisha ama ya shirikisha wanawake wanao ishi eneo za kazi katika ku kamata atuwa yaku linda hali ya hewa?	☐	☐

04 Hali ya maji

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha mara kwa mara hali ya maji kwa kila sehemu ya ufatiliyaji ama surveillance ?	☐	☐
b.	Ya julisha wakati gani na sehemu gani hali ya maji ina shuka chini ya mupaka ya usalama?	☐	☐
c.	Ya husisha ama ya shirikisha jamii zinayo ishi eneo za kazi katika ku kamata atuwa yaku linda hali ya maji?	☐	☐
d.	Ya husisha ama ya shirikisha wanawake wanao ishi eneo za kazi katika ku kamata atuwa yaku linda hali ya maji?	☐	☐

05 Wingi wa maji

	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha mara kwa mara, kiasi cha maji ambacho inatumia kutoka kwenye mazingira?	☐	☐
b.	Ya ongeya na jamii zinao ishi eneo za kazi ku usu namna yaku linda (Gérer) uwezo yaku fikilia maji inayo shirikiwa (partagé) ?	☐	☐
c.	Ya husisha kabisa wanawake katika maongezi ku usu namna yaku linda uwezo yaku fikilia maji inayo shirikiwa?	☐	☐
d.	Ya husisha jamii zinao ishi eneo za machimbo katika ku kamatata atuwa za ku punguza ku tumizi yake ya maji?	☐	☐

06	Kurejesha hali ya kawahida (ukarabati) ya eneo na shughuli baada za ku funga eneo yaku chimba madini		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya fanya yote ku julisha jamii za eneo ku husu ku shimamisha ao ku funga kazi za madini?	☐	☐
b.	Ya husisha ama ya shirikisha jamii katika mipango zake za kurejesha hali ya kawaida ya eneo kisha ku funga kazi za madini?	☐	☐
c.	Ya fanya yote ku juwa kama jamii za eneo zili itika mipango za kurejesha hali ya kawaida ya eneo kisha ku funga kazi za madini?	☐	☐
d.	Ya husisha kabisa wanawake ku tokeya jamii za eneo za kazi katika matayarisho na ku itika mupango za kurejesha hali ya kawaida ya eneo kisha ku funga kazi za madini?	☐	☐

07	Matumizi za mabaki (ao masaliyo)		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha kwa wote eneo inayo weka makabi ama masaliyo ku tokeya kazi za madini?	☐	☐
b.	Ya fanya yote kwaku fahamisha mahali mabaki ama masaliyo zime wekwa kwaku linda ulinzi ya watu na nyama?	☐	☐
c.	Ya julisha kwa wote eneo inayo weza guswa wakati kufungwa ya mabaki ama masaliyo ina shindikana ama kuharibika?	☐	☐
d.	Ya pima mara kwa mara ngunga ao namna za ku julisha kwa haraka wa fanyakazi na jamii za eneo za kazi wakati ku fungwa ya mabaki ama masaliyo ina shindikana ama kuharibika?	☐	☐

08	Usalama wa jamii		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha idadi na hali za vifo ambavyo hutokea katika eneo lake la kuchimba madini?	☐	☐
b.	Ya fanya yote ku julisha jamii za eneo nini ku fanya wakati kuna dharura/urgence inao usu machimbo?	☐	☐
c.	Ya husisha jamii ya eneo katika mapimo (test) za mipango zake za majibu kwa darhura?	☐	☐
d.	Ya husisha kikamilifu wanawake wa eneo katika mapimo (test) za mipango zake za majibu ya darhura/urgence ?	☐	☐

09	**Malalamiko ma manunguniko za jamii**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ili tiya mfumo ama njia ya malalamiko inayo weza saidiya jamii na watu wanayo ishi katika eneo za madini ku rekodi ama enregistrer malalamiko na manunguniko?	☐	☐
b.	Ya fanya yote kwaku tayarisha wafanyakazi wake wa kiume na wa kike wakuwe tayari kwaku pokeya na ku kutibu maunginiko za jamii ili wanawake wa jami katika eneo ya machimbo wa zungumuze na mwanawake?	☐	☐
c.	Ya julisha kwa wote idadi na haina za malalamiko/manunguniko zinayo rekodiwa na watu na jamii?	☐	☐
d.	Ya onegeya na jamii ku usu hatua zinayo chukuliwa ili kuepuka kutokea tena kwa malalamiko/manunguniko sawa izo?	☐	☐

10	**Usalama na afya za wafanyakazi**		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya gabula vifaa vya usalama vinavyo faa kwa wafanyakazi wake wote na watu wanaofanyia kazi ku pitiya wa sous-taitant, bila malipo?	☐	☐
b.	Ya jenga fasi za choo na za mavaliyo zenyi ku faa kwa wafanyakazi wake wote na wa fanya kazi kupitiya wa sous-traitant ?	☐	☐
c.	Ya hakikisha kuwa wafanyakazi wa kike wote wana uwezo wa kufikia fasi za choo na ya mavaliyo inayofaa na ziliyotengwa na zile zinayotumiwa na wafanyakazi wa ume?	☐	☐
d.	Ya julisha kwa wote saa za wastani (heures myennes) za kila mfanyakazi kufanya kazi na kwa siku?	☐	☐

11 Wafanyakazi wa kike			
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya kamata hatua za kuzuia unyanyasaji wa wafanyakazi wa kike?	☐	☐
b.	Ya kamata hatua za kuzuia vurugu za kijinsia (violation du genre) kwa wafanyakazi wa kike?	☐	☐
c.	Ya gabula nguo za kazi na vifaa vya ulinzi wa binafsi ambavyo vinafaa kwa miili ya wafanyakazi wake wa kike na wanawake wanaofanya kazi ku pitiya wa sous-traitant?	☐	☐
d.	Ya pana mafunzo ku usu jinsia kwa wafanyakazi wake wote na watu wanaofanyia kazi ku pitiya wa sous-traitant ?	☐	☐

12 Majeraha ama kulumiya na vifo inayo tokeya mahali pa kazi			
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya julisha kwa wote idadi na hali za ku lumiya na vifo ya wafanyakazi wake kutokeya mahali pa kazi?	☐	☐
b.	Ya julisha kwa wote idadi na hali za ku lumiya na vifo za wafanyakazi wa sous-taitant kutokeya mahali pa kazi?	☐	☐
c.	Ina comité mixte ya afya na usalama kazini iliyotungwa na wa wakilishi wa wafanyakazi na waajiri ili kuchunguza hatari na msiba?	☐	☐
d.	Ya hakikisha kuwa wafanyakazi wa kike wamewakilishwa kwenye comité mixte ya afya na usalama kazini?	☐	☐

13 Mafunzo ya wafanya kazi			
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya hakikisha kuwa wafanyakazi wake wote na ambao kufanya kazi ku pitiya wa sous traitant wanapokea maelekezo za lazima kwa kufanya kazi zao kwa usalama na kwa ku epuka ku lumiya?	☐	☐
b.	Ya toa mafunzo kwa wafanyakazi bila malipo, ili wa panuwe ujuzi wao wa kifundi?	☐	☐
c.	Ya hakikisha kuwa wafanyakazi wa kike wanaweza kufikia mipango yote ya mafunzo na bahati za kujifunza?	☐	☐
d.	Ya husisha wafanyakazi wake wote na ambao kufanya kazi ku pitiya wa sous traitant katika ku pima mipango zake za majibu za dharura?	☐	☐

14	Mshahara wa ku wezesha ku ishi maisha mazuri		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ya chunguza kiwango cha mshahara ambao wafanyakazi na familia zao wana itaji kwa ku kuishi maisha mazuri?	☐	☐
b.	Ya hakikisha kuwa mishahara ya wafanyakazi wake wote inafikia ao inazidi kiwango hiki cha mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri?	☐	☐
c.	Ya hakkikisha kuwa mishahara ya watu wote ambao hufanya kazi ku pitiya wa sous-traitant pia inafikia au inazidi kiwango hiki cha mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri?	☐	☐
d.	Ya julisha kwa wote kiwango cha mshahara wa chini zaidi kwa wafanyakazi wa kiume na wa kike kwa kila kiwangocha kazi?	☐	☐

15	Malalamiko na maunguniko za wafanyakazi		
	Kwa eneo hili la kuchimba madini, je kampuni:	HAPANA	NDIYO
a.	Ina mupango ya kushughulikia manunguniko ya wafanyakazi wake na watu wanaofanya kazi ku pitiya wa sous-traitant kwa ku rekodi malalamiko/manunguniko?	☐	☐
b.	Ya hakikisha kuwa wafanyakazi wa kiume na wa kike wanapatikana ili kupokea na ku chunguza manunguniko ya wafanyakazi ili wafanyakazi wa kike waweze kuzungumza na mtu wa jinsia sawa na yao?	☐	☐
c.	Ya julisha kwa wote idadi na aina ya malalamiko/manunguniko ziliyo rekodiwa na wafanyakazi wake na watu wanaofanya kazi ku pitiya wa sous-traitant ama kampuni saidizi?	☐	☐
d.	Ya ongeya na wafanyakazi wake, wafanyakazi za wa sous-traitant na wawakilishi wao kuhusu hatua zinazo chukuliwa ili kuepuka kutokea tena ya malalamiko/manunguniko sawa izo?	☐	☐

Maoni:

Kuhusu

01 Ku usu wafanyakazi wana mujini

Kampuni ambayo ina julisha watu ngapi wanaoishi katika eneo ambao kufanyia kazi katika eneo lake la kuchimba madini inaweza kuonyesha kujitolea kwake katika kujiweka kwenye maendeleo ya jamii za eneo hilo. Hatua ya ku julisha kuhusu wafanyakazi wa kike huisaidia kampuni kuonyesha kuwa hakuna ubaguzi katika ujaguzi (discrimination) ya wafanya kazi wa kike. Kampuni inaweza kutoa picha kamili zaidi ya hali ya ajira kwa kuonyesha watu ngapi wanaoishi katika eneo za machimbo ambao wanafanyia kazi ku pitiya wa sous-traitant.

02 Ku nunuwa kwenyi eneo

Kampuni ambayo hununua vifa via kazi ndani ya eneo ya machimbo inaweza kuchangia ukuaji wa biashara na ukuaji wa uchumi katika eneo. Kampuni inapotoa maelezo kuhusu kupata vifaa vya eneo, inasaidia biashara ya eneo kutambua fursa za kuwa wasambazaji wa bidhaa na huduma kwa eneo la kuchimba madini na inaonyesha pia jinsi inavyohimiza biashara za eneo kuwa wasambazaji wa bidhaa na huduma.

03 Hali ya hewa

Uchafuzi wa hewa ni wasiwasi mkubwa kwa jamii nyingi zinazo guswa na kuwepo kwa eneo la kuchimba madini, kwa sababu uchafuzi wa hewa unaweza hatarisha afya zao, mimea yao ya chakula, mifugo yao na wakati mwingine pato yao ya kuishi. Kampuni ina julisha data kuhusu ubora wa hewa karibu na eneo la kuchimba madini na kujadiliana na jamii kuhusu jinsi inavyodhibiti ubora wa hewa, inaweza kujenga imani na kupunguza hofu inayohusiana na vumbi na uchafuzi wa hewa.

04 Hali ya maji

Kampuni inaweza kufanya maelezo yake ya umma kuhusu ubora wa maji yawe ya manufaa zaidi kwa jamii husika kwa ku julisha mara kwa mara data ya ubora wa maji katika kila sehemu ambako inakusanya data kama hiyo. Kampuni pia inaweza kujenga imani kwa kubainisha mahali na wakati ambapo ubora wa maji ulipunguka chini ya mipaka ya usalama na kwa kujadiliana na jamii ya eneo atuwa ambayo ina chukua ili kudhibiti ubora wa maji.

05 Wingi wa maji

Uwezo wa kufikia maji ina weza kuwa mwanzo ya migogoro kati ya kampuni za kuchimba madini na jamii za eneo, hasa katika maeneo yaliyo na uchache wa maji. Kampuni inaweza kuonyesha heshima yake kwa jamii za eneo kwa kufichua kiasi cha maji inachotumia kutoka kwa vyanzo vya eneo na kwa kujadiliana na jamii za eneo jinsi matumizi yake ya maji yanavyo zingatia mahitaji ya maji ya watu wanaoishi katika eneo hii.

06 Kurejesha hali ya kawahida (ukarabati) ya eneo na shughuli baada za ku funga eneo yaku chimba madini

Ili kampuni iweze kuacha matokeo mazuri kwenye eneo lililo karibu na eneo lake la kuchimba madini, inahitaji kuhakikisha kuwa jamii ya eneo zitakuwa na mapato ya kudumu eneo la kuchimba madini litakapofungwa. Hii inajumuisha kuhakikisha kuwa watu wanaoishi katika eneo wataweza kutegemea rasilimali asili zenye ubora wa juu (udongo, maji nk.) na uwezekano za kibiashara. Kampuni pia itahitaji kujadili na kuidhinisha mpango wa kufungwa kwa eneo la kuchimba madini na jamii za eneo ili kuzingatia jinsi watu wanaoishi katika eneo hii wanavyo taka eneo lionekane baada ya eneo la kuchimba madini kufungwa.

07 Matumizi za mabaki (ao masaliyo)

Barrage ya mabaki yanaweza kuwa hatari zaidi kwa watu, mifugo na mazingira. Iwapo barrage ya mabaki yatavunja kingo zake, yanaweza kuachilia kiasi kikubwa cha uchafu ambao unaweza kusababisha vifo, kufunika mitoni, kuzika manyumba, kuharibu mapato na ku haribu vibaya sana mazingira na jamii za eneo kwa miaka mingi ijayo. Kampuni inaweza kuonyesha kuwa inachukulia suala hili kwa uzito zaidi kwa kufichua maelezo yanayoweza kutekelezwa kwenye barrage zake za mabaki, kwa kuhakikisha kuwa barrage haya yametiwa sahihi kwa njia dhahiri na kufanywa kuwa salama ili kuzuia majeraha ya ajali au vifo vya watu na wanyama na kwa kujaribu mara kwa mara mifumo yaonyo.

08 Usalama wa jamii

Kwa kawaida ku chimba madini ni hatari kwa jamii za eneo za machimbo, kwa sababu ajali na migogoro inaweza kusababisha vifo na majeraha. Kampuni inaweza kuheshimu jamii ya eneo na kusaidia kudumisha usalama wao kwa ku julisha idadi na hali za vifo yoyote ambavyo vinatokea. Ata kama ni vigumu kutoa hakikisho kuwa hali za dharura zinazohusiana na uchimbaji wa madini hazitawayi kutokea, kampuni inaweza kupunguza athari zozote mbaya kwa kubuni mipango ya kudhibiti dharura na hali ya hatari. Kwa kuhusisha wanachama wa jamii katika kujaribu mipango hii ya kukabiliana na hali, kampuni zinaweza kusaidia kuhakikisha kuwa mipango inafanya kazi vizuri iwapo hali ya dharura ya kweli itatokea.

09 Malalamiko ma manunguniko za jamii

Kampuni ambayo inaheshimu jamii ya eneo kutaka kufahamu na kushughulikia masuala yao. Hii inajumuisha kubuni mchakato rasmi (unaoitwa mbinu ya kushughulikia manunguniko ya jamii) ambao unawawezesha watu au makundi kutoka kwa jamii za eneo kuwasilisha malalamiko yao, ili masuala haya yasuluhishwe na kampuni. Kuna uwezekano kuwa wanajamii wataamini na kutumia mbinu hizi za kuwasilisha malalamiko iwapo kampuni julisha jinsi ambavyo mbinu inatumika na hatua ambazo zinachukuliwa ili kuhakikisha kuwa malalamiko yanashughulikiwa kwa njia bora.

10 Usalama na afya za wafanyakazi

Mazingira salama ni yale ambayo yanadumisha afya ya mwili na ya kiakili ya wafanyakazi. Mazingira safi ya kufanyia kazi kwa kawaida huwa yenye tija zaidi na maeneo ya kuchimba madini yenye hali nzuri za usalama yana fursa nzuri ya kuvutia wafanyakazi na wawekezaji. Kampuni ya kuchimba madini inaweza kuepuka na kupunguza hatari za usalama kwa kuwapa wafanyakazi wake vifaa vinavyofaa vya kujikinga na vyoo vinavyofaa na vifaa vya kuoshea mikono ambavyo ni salama kwa wanaume na wanawake. Kufuatilia ratiba za kazi kwa uwazi kunaweza pia kuzuia tabia za unyanyasaji zinazowezakutokea.

11 Wafanyakazi wa kike

Wafanyakazi wa kike wako katika hatari zaidi katika hali za kufanya kazi ambazo si salama na hazifai. Kampuni inaweza kuonyesha heshima yake kwa wafanyakazi wa kike kwa kuchukua hatua za kuzuia unyanyasaji na vurugu za kijinsia (violation du genre), pamoja na kuwapa wanawake nguo zinazofaa za kufanyia kazi na vifaa vya kujilinda. Mafunzo yanayofaa ni muhimu ili kuwasaidia wanawake na wanaume kuelewa jukumu la jinsia na kuboresha usawa wa kijinsia mahali pa kazi.

12 Majeraha ama kulumiya na vifo inayo tokeya mahali pa kazi

Uchimbaji madini ni kazi hatari. Ajali hatari zaidi zinazotokea katika maeneo ya kuchimba madini bado zinaendelea kutokea duniani kote. Kampuni ya kuchimba madini inaweza kuepuka na kupunguza hatari za usalama wa mahali pa kazi kwa kufichua na kufanya uchunguzi wa ajali na vifo. Sekta ya uchimbaji wa madini inategemea zaidi wakandarasi ama sous-traitants, kwa hiyo ni muhimu kwa kampuni pia kutoa maelezo kuhusu vifo vyovyote vya watu wanaofanya kazi kwa wakandarasi (sous-traitants), ili kutoa picha kamili zaidi ya hali ya usalama wa wafanyakazi wake.

13 Mafunzo ya wafanya kazi

Kulingana na Shirika la Kimataifa la wafanyakazi, hakuna mtu yeyote anayepaswa kuajiriwa ili kufanya kazi katika eneo la kuchimba madini isipokuwa mtu huyo awe amepokea mafunzo na maagizo yanayohitajika ya kumwezesha kufanya kazi kwa bidii na kwa usalama. Kwa hiyo, mafunzo hayapaswi tu kuzingatia afya na usalama na mbinu za kukabiliana na dharura, lakini pia ujuzi wa kiufundi. Hatua ya kuelimisha na kufunza wafanyakazi inaweza kusababisha kuwa na jopokazi lenye tija zaidi

14 Mshahara wa ku wezesha ku ishi maisha mazuri

Mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri ni ule ambao unawawezesha wafanyakazi na familia zao kumudu maisha ya msingi lakini ya kisasa, kuishi juu ya kiwango cha umaskini na kuweza kushiriki katika maisha ya kijamii na kitamaduni. Mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri ni haki ya msingi. Kampuni ya kuchimba madini ambayo huchukua hatua ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wake na watu wanaofanya kazi ku pitiya wa sous-traitant wanalipwa mshahara wa kuwezesha kuishi maisha mazuri inaweza kuimarisha uhusiano wake na wafanyakazi, kuboresha zamiri na kazi ya wafanyakazi; na kuonyesha kuwa inaheshimu haki za wafanyakazi wake.

15 Malalamiko na maunguniko za wafanyakazi

Kampuni ambayo inaheshimu wafanyakazi wake hutaka kufahamu na kushughulikia masuala yao. Ni ku tiya mchakato (unaoitwa mbinu ya kushughulikia manunguniko ya wafanyakazi) ili kuwapa wafanyakazi njia ya kuwasilisha malalamiko ili masuala yao yanaweze kushughulikiwa na kampuni. Mbinu bora ya kushughulikia manunguniko itasababisha kuwepo kwa mahusiano mazuri kati ya kampuni na wafanyakazi lake. Kampuni inaweza kuendeleza imani kwenye mchakato wa kushughulikia manunguniko kwa ku julisha jinsi mbinu ya kushughulikia manunguniko inavyotumika na jinsi kampuni inavyochukua hatua ili kuhakikisha kuwa malalamiko yanashughulikiwa kwa njia bora.

Ili upate utaratibu kamili wa masuala yanayohusiana na uchimbaji madini wa kuwajibika, unaweza kutembelea tovuti ya Responsible Mining Foundation:
www.responsibleminingfoundation.org

Kwa maswali na usaidizi, tafadhali tuma barua kwa
contact@responsibleminingfoundation.org

Dokezo
Maudhui ya hati hii hayawakilishi maoni ya wafadhili, wadhamini na wafanyakazi wa Responsible Mining Foundation (RMF) na wengine walioshiriki katika mashauriano na waliohudumu kama washauri kwa hati hii.

Imechapishwa bila malipo kama bidhaa ya umma
Data na maudhui yote yaliyoandikwa yamepewa leseni chini ya Leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-NonCommercial 4.0 (CC BY-NC 4.0). Watumiaji wako huru kushiriki na kutumia nyenzo hii lakini ni lazima watoe shukrani kwa wahusika, watoe kiungo cha kuelekeza kwenye leseni na waonyeshe iwapo mabadiliko yalifanywa. Nyenzo iliyopewa leseni haipaswi kutumiwa kwa madhumuni ya kibiashara au kwa njia ya kubagua, kudhalilisha au kupotosha ukweli. Inapotajwa, ihusishe na: «Responsible Mining Foundation (RMF) (2020), '*Chombo cha uchunguzi ya eneo ya ku chimba madini*'»